**JAMHURI YA MUUNGO WA TANZANIA**

**BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA**

**MTIHANI WA UALIMU DARAJA LA A**

**634** **STADI ZA KAZI**

**Muda: Saa 3 Hours** **Mwaka: 2024**

---

**Maelekezo**

1. Karatasi hii ina Sehemu **A** na **B** zenye jumla ya maswali **kumi na manne (14).**
2. Jibu maswali **yote** kutoka Sehemu **A** na maswali **manne (4)** kutoka Sehemu **B**.
3. Sehemu **A** ina alama **arobaini (40)** na Sehemu **B** ina alama sitini **(60).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** ndani ya chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

maktaba.tetea.org
TETEA


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

1. Bainisha hatua nne za kuzingatia wakati wa ufuaji wa nguo za pamba.
2. Ainisha kwa ufupi mbinu nne za uimbaji wa nyimbo.
3. Bainisha sababu nne za walimu wa somo la Stadi za Kazi kufundisha kwa kutumia msingi wa Ubunifu, Uundaji, Utungaji na Ufaraguzi.
4. Eleza kwa kifupi hatua nne zinazotakiwa kufuatwa katika kuanzisha biashara ndogo ndogo.
5. Eleza kwa kifupi hatua nne zinazofuatwa wakati wa kurekebisha sehemu ya juu ya kiatu.
6. Eleza kwa kifupi mambo manne yatakayozingatiwa na mwalimu katika kutumia njia ya ziara kufundisha mada ya Kilimo na Ufugaji kwa wanafunzi wa Darasa la Sita.
7. Kufafanua kwa kifupi namna ya kuandaa juisi ya machungwa.
8. Ainisha fani zinazopatikana katika sanaa za maonesho ambazo zinatambulisha na kuimarisha utamaduni wa Tanzania.
9. Eleza kwa ufupi vifaa vinne vinavyotumika kutengeneza kofia na matumizi ya kila kifaa.
10. Eleza faida nne za kutumia mbinu ya majadiliano katika ufundishaji wa mada ya Upishi.

## SEHEMU B (Alama 40)

Jibu maswali **yote** katika sehemu hii.

11. Eleze umuhimu wa upimaji baada ya kukamilisha ufundishaji wa somo la Stadi za Kazi.
12. Fafanua umuhimu wa kutumia andalio la somo wakati wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Stadi za Kazi.
13. Chambua faida sita za kutumia mbolea za asili katika kuzalisha mazao ikilinganishwa na zile za viwandani.
14. Eleza faida sita za mada ya Usanii wa Picha, Chapa, Maumbo na Mapambo katika muhtasari wa somo la Stadi za Kazi.


Find this and other free resources at: https://maktaba.tetea.org